*JARIDA LA CHALUFAKITA*
*Juz. 4, 2022, 93 -104*

# MCHANGO WA KASIDA TEULE ZA ZANZIBAR KATIKA MAPAMBANO DHIDI YA UGONJWA WA VIRUSI VYA KORONA

Ulfat Abdul-aziz Ibrahim
Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar-Tanzania
madamullu@gmail.com /director.zls@moez.go.tz

*DOI: https://dx.doi.org/10.4314/jclfkt.v4i1.7*

**Ikisiri**

*Kasida kama aina mojawapo ya nyimbo zenye maudhui ya kidini zimekuwapo katika jamii zetu kwa muda mrefu. Kasida hizi hutumika katika matukio mbalimbali ya kijamii kama vile sherehe na misiba (Said, 2016). Kupitia kasida, jamii imekuwa ikielimika, kuburudika na kupata nasaha muhimu za maisha. Aidha, kwa kuwa kazi za sanaa, ikiwamo fasihi, ni zao la jamii, watunzi wa kasida za kidini pia husukumwa na matukio mbalimbali ya kijamii kutunga kazi zao. Kwa muktadha huo, makala hii inalenga kuchambua mchango wa kasida za dini katika mapambano dhidi ya Ugonjwa wa Virusi vya Korona– 19 (kuanzia sasa UVIKO-19). Ili kusheheneza makala, mwandishi amesikiliza na kuchambua kasida teule zilizoimbwa kutoka vikundi na madrasa teule za Zanzibar. Ukusanyaji data na uchambuzi wake umeongozwa na Nadharia ya Uhalisia. Matokeo ya utafiti yameonesha kuwa kasida zina mchango mkubwa kwa jamii. Miongni mwa mchango huo ni pamoja na kukumbusha watu kumrejea Mungu, kutoa elimu ya kujikinga na UVIKO-19, kueleza hali ya upatikanaji wa huduma za afya, kubainisha athari za UVIKO-19 na kufanya maombi juu ya kutokomeza UVIKO-19. Kwa ujumla, makala imebainisha mchango wa kasida teule kwa jamii ya Wazanzibari, hususani katika kupambana na magonjwa ya mlipuko. Hivyo, mwandishi anapendekeza kuwa jamii iziendeleze kasida katika kutoa elimu ya kuikinga, kupunguza athari na kuifariji jamii dhidi ya magonjwa mbalimbali ya mlipuko ukiwemo UVIKO-19.*

## 1.0 Utangulizi

Kasida hufafanuliwa kama kipera kimojawapo cha nyimbo kinachofungamana na maudhui ya dini. Nyimbo hufasiliwa kuwa ni aina ya fasihi ambayo hutumia lugha teule, sauti na kiimbo maalumu. Aghalabu, nyimbo hutumia ala za muziki kama vile ngoma, filimbi, gitaa na piano. Mulokozi (2017) anaongezea kuwa wimbo ni utungo wa kisanaa unaowasilishwa kimuziki kwa kutumia sauti iliyo katika mpangilio fulani wa mahadhi na melodia na wenye mapigo ya kiurari. Nyimbo zinaweza kuimbwa na mtu mmoja, wawili au hata kundi la watu. Kwa kawaida, nyimbo hugawanywa katika beti, mishororo na kiitikio au mstari ambao hurudiwarudiwa.

Kwa mujibu wa Finnegan (1970), tanzu za nyimbo zinaweza kutofautiana katika muundo, mtindo, maudhui na dhima, lakini zina kitu kimoja ambacho huzifanya zote zifanane ambacho ni usimulizi. Kutokana na tofauti hizo, Finnegan (khj) ameziweka nyimbo katika makundi mbalimbali. Miongoni mwa makundi hayo ni nyimbo za dini (zikiwamo kasida), nyimbo za jadi na nyimbo za watoto. Pia, nyimbo hutofautiana maudhui kutokana na muktadha uliofungamana na utunzi wake. Kwa mfano, zipo nyimbo zinazohusiana na ibada (imani za kidini), sherehe na kilio. Wamitila (2003) anaona kuwa nyimbo zina sifa zifuatazo: sauti ya mwimbaji, ala au vyombo vya muziki, matini au maneno yanayoimbwa, hadhira inayoimbiwa, kuimbwa na mtu mmoja au watu wengi, matumizi ya lugha ya mkato, na kurudiarudia (kukariri).

Kama zilivyo tanzu nyingine za fasihi, nyimbo zina dhima muhimu kwa jamii. Miongoni mwa dhima hizo ni kuburudisha, kuelimisha na kuliwaza. Tunaposikiliza ala, mpangilio maalumu wa maneno unaojikita katika vina na mizani, bila shaka mioyo ya wasikilizaji hupata faraja na kusuuzika na hivyo kuwa burudani kwa wasikilizaji. Aidha, yale yanayosemwa kupitia wimbo mara nyingi hulenga kutoa elimu kwa jamii kuhusu mambo mbalimbali. Hii ni kusema kuwa, nyimbo ni sanaa muhimu inayoweza kutoa elimu kwa jamii kuhusu athari za vitendo vibaya kama vile wizi, uzinzi, ubakaji, ulevi, usengenyaji na maradhi. Pia, nyimbo ni kiliwazo cha jamii, hasa katika mazingira ya shida, kadhia na majanga. Katika hali hizi, maneno ya wasanii kupitia nyimbo huleta faraja kwa jamii na kuwa kitulizo chema kwa wanajamii wanaosikiliza. Uchunguzi uliozaa makala hii uliangalia mchango wa kasida teule za Zanzibar katika mapambano dhidi ya UVIKO-19.

Katika kufasili dhana ya kasida, BAKIZA (2010) linaeleza kuwa kasida ni shairi aghalabu lenye maudhui ya kumsifu Mtume Muhammad (S.A.W), kuusia watu na kufunza maadili mema. Naye, Said (2016) anaeleza kuwa kasida ni mfumo wa sauti/ridhimu zinazotumika katika kumsifu Allah (S.W) na Mtume Muhammad (S.A.W). Anaendelea kueleza kuwa kasida kwa asili yake ina lengo la kujenga ustawi wa alaka (tabia njema) na kuimarisha uhusiano kati ya mja na Muumba wake. Kwa mujibu wa Mulokozi (2017), kasida na nyimbo nyingine za dini zinahusu mafunzo ya dini kama vile kumtambua Mungu, ibada, dhambi, mauti, akhera, mitume na viongozi wa dini, sambamba na mahusiano mema baina ya waumini. Kwa kutazama maelezo ya fasili zote, kuna mambo matatu yanayoshadidiwa. Mosi, kasida ni utungo au maghani ya kishairi. Pili, kasida zinafunza mambo muhimu ya dini ya Kiislamu. Mafunzo hayo yanahusu kumjua Mungu na Mtume wake. Tatu, kasida zinalenga kustawisha tabia njema miongoni mwa wanajamii.

Katika kuziweka kasida katika makundi mbalimbali, Said (2016) amezigawanya kasida kwa kigezo cha kimaudhui. Kupitia makundi hayo kuna kasida za harusi,

kasida za tanzia, kasida za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, kasida za uradi, kasida za Twariqa, kasida za Maulidi ya homu na kasida za matukio. Kasida za harusi ni zile kasida ambazo husomewa wakati bi harusi anapoolewa au bwana harusi anapooa kwa lengo la kusherehekea ndoa yake, kuwapongeza, kuwashangilia na pia kutoa mafunzo juu ya maisha ya ndoa. Kasida za tanzia ni zile ambazo zinasomwa kwa huzuni au masikitiko juu ya jambo fulani lenye kuhuzunisha. Mfano wa kasida hizi ni zile zinazoimbwa katika misiba. Kasida za uradi ni zile ambazo zinasomwa kwa lengo la kumfunza mwari wakati anapotaka kuolewa ikiwamo kutunza nyumba yake, kuwaheshimu wazazi wa mume (wakwe), mawifi, shemeji na hata majirani. Kasida za Twariqa ni zile zinazosomwa kwa dhikri (utajo wa Allah). Kasida hizi husomwa na vikundi vya watu wazima kutoka maeneo mbalimbali, hususani vijijini. Kwa mfano, kuna Twariqa ya Tumbatu (Unguja) na Muambe (Pemba). Kasida za matukio husomwa baada ya kutokea matukio fulani maalumu katika jamii. Mara nyingi, matukio hayo huwa makubwa na yanayoigusa jamii pana. Mifano ya kasida hizo ni zile zilizohusiana na kuzama kwa meli ya 'M.V Spice Islanders', janga la kulipuka kwa mabomu ya Mbagala (Dar es Salaam) na milipuko ya maradhi ya UKIMWI, ndui, ukoma, kipindupindu na UVIKO-19.

Katika makala hii, mwandishi amechunguza mchango wa kasida teule za Zanzibar katika mapambano dhidi ya mlipuko wa UVIKO-19. Mlipuko wa Ugonjwa wa Virusi vya Korona ulitangazwa rasmi na Shirika la Afya Duniani (WHO) mnamo Januari 2020. Ugonjwa huo uligundulika katika mji wa Wuhan, Jimbo la Hubei, nchini China. Baada ya kipindi kifupi cha miezi mitatu, Korona ilisambaa duniani kote na kutangazwa kuwa janga la kimataifa. Kwa mujibu wa WHO (2021), mpaka kufikia Aprili 2, 2020 (yaani miezi mitatu tu tokea kugundulika kwa UVIKO-19), watu takribani 896,450 walikuwa wameambukizwa UVIKO-19 katika nchi zaidi ya 200. Aidha, ugonjwa huo ulisababisha vifo vya watu maelfu kadhaa duniani kote. Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, maambukizi ya ugonjwa huu yaliripotiwa katika nchi za Burundi, Kenya, Rwanda, Uganda na Tanzania (WHO, 2021). Kwa Tanzania, serikali ilifanya juhudi kubwa ya kuelimisha jamii kupitia vyombo vya habari kuhusiana na ugonjwa huu. Aidha, serikali ilihimiza wadau mbalimbali kuunga mkono juhudi zake kwa kutoa elimu kwa jamii ili kupunguza kasi ya kuenea UVIKO-19 (MOHZ, 2022).

Kutokana wito wa serikali, wadau wa kazi za fasihi na sanaa nyingine waliungana na serikali kuelimisha jamii kuhusu Korona. Kwa upande wa Zanzibar (ambayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania), wasanii wa kasida waliitikia wito wa serikali na kupitia kazi zao walisaidia sana kutoa elimu kwa umma kuhusu Korona. Kwa kuzingatia ukweli kuwa kasida ni miongoni mwa sanaa zinazopendwa visiwani Zanzibar, mchango wa watunzi wa kasida unapaswa kuchunguzwa na kujadiliwa (Said, 2016). Hivyo basi, mwandishi wa makala hii

alichunguza mchango wa kasida za Zanzibar katika kutoa elimu kwa umma kuhusu ugonjwa wa UVIKO-19.

## 2.0 Mkabala wa Kinadharia

Makala hii imeongozwa na Nadharia ya Uhalisia. Nadharia ya Uhalisia ni moja ya mikabala ya kisosholojia inayosisitiza uhusiano na mfungamano uliopo kati ya fasihi na jamii, na kwamba kazi ya fasihi ni zao halisi la jamii mahususi (Mulokozi, 2017). Nadharia hii iliibuka Ulaya miaka ya 1850 ili kupinga Uromansia na kusisitiza kwamba fasihi inapaswa kuyasawiri maisha kama yalivyo bila kupotosha, wala kutia chumvi. Nadharia hii ilijikita katika kuonesha mahusiano na migongano ya kijamii, na matatizo na matamanio ya mtu wa kawaida katika hali ya kawaida ndani ya jamii (Ntarangwi, 2004 na Mlaga, 2017). Kazi za kifasihi zinazolengwa kuchunguzwa kwa mwongozo wa nadharia hii ni zile zinazochunguza na kuyachanganua masuala ya kawaida, hata yawe madogo, ilimradi yanamhusu mhusika na maisha yake binafsi, tabaka lake na jamii yake katika mandhari na mazingira yake.

Ntarangwi (2004) akimnukuu Jules Husson Champfleury (1821-1889) anaeleza kuwa ‘nyenzo ya uhalisia ni uwakilishaji wa maisha ya kila siku ya jamii inayohusika’. Nadharia ya Uhalisia inajitokeza katika kazi mbalimbali za fasihi. Uhalisia katika kazi za fasihi huashiria uwezo wa kusawiri au kuelezea hali kwa kuzingatia uyakinifu au uhakiki wa maisha. Uhalisia pia hujihusisha na uigaji wa mazingira anamopatikana mwanadamu (Wafula na Njogu, 2007). Kama nadharia, uhalisia huzingatia namna ukweli unavyosawiriwa katika nyakati na vipindi mbalimbali. Jinsi ya kuusawiri au kuuelewa uhalisia hutofautiana kutoka jamii hadi jamii, na kutoka kipindi kimoja cha kihistoria hadi kingine. Kila kizazi kina uhalisia wake ambao huweza kusawiriwa kifasihi. Fasihi inaweza kusawiri uhalisia wa wakati ujao kwa kutumia wakati uliopo. Fasihi inaweza kusawiri uhalisia kwa kutumia ubunifu unaoongozwa na misingi ya kisayansi. Fasihi inaweza kusawiri uhalisia kwa kutumia ubunifu unaoongozwa na misingi ya historia.

Nadharia ya uhalisia huelezea kazi ya fasihi inayowasilisha ulimwengu wa maisha ya kijamii yenye wahusika wanaotenda mambo yanayodhibitiwa na hali ambayo wahusika hao wamo. Huwakilisha uhalisi wa mambo ya kijamii katika fasihi. Mwanauhalisia huamini kuwa matokeo ya mambo na ukweli anaouzingatia ni ule unaoweza kuonekana na kuthibitishwa kwa tajiriba za wanajamii. Huiamini demokrasia kama hali ya maisha, na malighafi anayochagua msanii kuyaeleza maisha ni yale maisha ya kawaida, ya kadiri na ya kila siku. Husisitiza usawiri wa uhalisi katika ukamilifu wake na kwamba yanayoshughulikiwa hayana budi kuthibitika. Kwa hiyo, mchango mkubwa wa nadharia hii ni kuyachora maisha kama yalivyo. Pamoja na msanii kujizatiti kuchora hali halisi ya maisha kama yalivyo, hutetea watu fulani na kuwashambulia wengine kutegemea msimamo

wake (Wafula na Njogu, 2007). Hivyo basi, uhalisia hujikita katika mambo yaliyopo, matukio mahususi na matokeo yanayoweza kuthibitika. Imani ya mwanauhalisia ni kwamba, kazi ya fasihi inapaswa kuwaweka wanajamii husika katika ulimwengu wao wa kawaida, wa kweli, na halisi.

Kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007), nadharia ya uhalisia ina misingi ifuatayo: (a) Msanii hujitahidi 'kuyachora' maisha jinsi yalivyo bila kuathiriwa; na hufanya hivyo kupitia vipengele muhimu vya maisha kama vile siasa, uchumi, utamaduni, jamii, n.k.; (b) Wahusika husawiriwa wakiwa wa kawaida, huku wakiwakilisha jamii zao; (c) Lugha huwa ni ya kawaida, ikitumiwa na wahusika kama ilivyo katika maisha ya kila siku; (d) Mandhari na matukio inafaa yawe ni yale yanayoonekana, yanayojulikana au yanayowezekana. Inafaa mambo hayo yaendane na jamii husika; (e) Msanii huangalia matatizo ya jamii na kuchunguza chanzo chake. Hivyo, msanii huchunguza mabadiliko ya kihistoria ambayo husababisha hali mbalimbali za maisha, ikiwa ni pamoja na kuathiri mifumo ya fikra. Katika muktadha wa makala hii, misingi (a) na (e) imetumika zaidi. Misingi hiyo ilimuongoza mwandishi wa makala hii katika kuchambua data kuhusu kasida za Zanzibar na kuonesha mchango wake katika mapambano dhidi ya UVIKO-19.

## 3.0 Methodolojia ya Utafiti

Makala hii imetokana na utafiti wa maktabani uliofanyika Zanzibar kati ya mwezi Machi hadi Juni 2022. Data za makala hii zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji ambapo mwandishi alitazama na kusikiliza video za kasida na kunakili maudhui ya kasida hizo. Kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa, mwandishi aliteua video 18 za kasida zenye maudhui ya UVIKO-19 ambapo baadhi ya video hizo zimenukuliwa kama mifano ya data ya uchunguzi huu. Miongoni mwa video zilizonukuliwa katika data za makala hii ni *Korona* (Ismail, 2021), *Korona* (Issa, 2021), (M'barouk, 2021) *Turejee kwa Allah* na *Korona* (Shekhe 2022). Video za kasida hizo zilipatikana kupitia mtandao wa kijamii wa *YouTube*. Mwandishi alifanya uchambuzi wa kasida hizi kwa mujibu wa malengo ya makala yake. Data zilichambuliwa kimaelezo kwa kutumia mkabala wa kitaamuli ambapo alichambua data za maudhui alizozikusanya kutoka katika video.

## 4.0 Mchango wa Kasida Teule za Zanzibar Dhidi ya UVIKO-19

Katika sehemu hii mwandishi anabainisha na kujadili mchango wa kasida katika mapambano dhidi ya UVIKO-19. Kupitia uchambuzi wa data zilizokusanywa mwandishi ameweza kubaini mchango wa kasida teule kama ifuatavyo:

### 4.1 Kukumbusha Watu Kumrejea Mungu

Kukumbusha watu kumrejea Mungu baada ya kufanya makosa mbalimbali ya kibinadamu ni moja kati ya mchango wa kasida teule za Zanzibar kuhusu UVIKO-19 uliobainika katika makala hii. Ni dhahiri kuwa lilipoanza janga la UVIKO-19,

kulikuwa na hofu kubwa iliyotanda katika mioyo ya watu kote duniani. Pamoja na hofu hiyo, wapo pia walioamini kwamba, ugonjwa umekuja kama alama ya kuwakumbusha wanadamu kumuabudu Mungu. Haya yanathibitishwa na Mbarouk (2021) kupitia kasida iitwayo "*Turejee kwa Allah*" kwa kusema yafuatayo:

> "Dalili nyingi za wazi, huwa zinatokezea
> Kama kupatwa kwa mwezi, hata kupatwa kwa jua
> Pia na haya maradhi, yanotoka na kungia
> Atukumbusha Mwenyezi, maasi kuyakemea
> Huu wetu mtihani tumeletewa, turejee kwa Manani Mola Jalia
> Tupo tu mtihani tumeletewa
> Turejee kwa Manani Mola Jalia x 2

Katika ubeti huo, msanii anabainisha matukio kama vile kupatwa kwa mwezi na kupatwa kwa jua ambayo anaeleza kuwa huwa yanatokea ili yawe ukumbusho kwa jamii juu ya kurudi kwa Mola wao. Aidha, hoja ya kuwarejesha watu kwa Mungu ilienda sambamba na kuwakumbusha kuwa Mola Muumba yupo na wasisahau kufuata maamrisho yake. Kutokana na kujisahau huko, jamii imebadilika kutoka katika misingi ya kumridhisha Mungu na kwenda upande wa kumridhisha shetani. Katika muktadha huo, wako walioamini kuwa ugonjwa huu umeletwa na Mungu ili kumkumbusha mwanadamu juu ya yale anayoyafanya. Kupitia ubeti hapo juu, msanii amebainisha wazi kuwa maradhi yanayozuka (kwa wakati huo UVIKO-19) ni mtihani kutoka kwa Mungu na kuwa mtihani huo unatokana na wanadamu kuacha kumuabudu Mungu.

Kwa hiyo, nadharia ya uhalisia kupitia msingi (e) unaoeleza kwamba msanii huangalia matatizo ya jamii na kuchunguza chanzo chake, imetuwezesha kubaini kuwa msanii huangalia matatizo ya jamii na kuchunguza chanzo chake. Huchunguza mabadiliko ya kihistoria ambayo husababisha kubadilika hali mbalimbali za maisha, ikiwa ni pamoja na kuathiri mifumo ya fikra. Hii imetokea kutokana na msanii kuonesha kuwa majanga na mabalaa mbalimbali yanayotokea katika jamii yanasababishwa na wanajamii kukengeuka maagizo ya Mungu, hivyo, UVIKO-19 umetokea kama ukumbusho. Kwa hiyo, msanii anatoa rai kwa jamii kurudi kwa Mola wao ili waweze kuepushwa na maradhi na majanga mengine ya kimaisha.

## 4.2 Kutoa Elimu ya Kujikinga na UVIKO-19

Katika kutoa elimu, kasida huwafunza na kuwaongoza wanajamii kufanya mambo ambayo yatawafanya waishi maisha mazuri na salama. Elimu inayotolewa huwasaidia wanajamii kujikinga na maradhi pamoja na kuchochea ushirikiano kwa

jamii katika kujinga na magonjwa mbalimbali. Msanii Issa (2022) anabainisha hayo katika kasida iitwayo *Korona* amesema:

> Jema tufuateni, ushauri wa wana afiya
> Na tupunguzeni, mkusanyiko, tunojifanyia
> Na tujue wazi, dawa haijapatikana
> Kinga bora vazi, kosha mikono yako vyema

Katika ubeti huo ni wazi kuwa msanii anaeleza kuwa ugonjwa upo hadi sasa na kuitahadharisha jamii kuwa ugonjwa huo haujapatiwa dawa. Kuhusu elimu ya kujikinga na ugonjwa wa UVIKO-19. Aidha, katika kasida hiyo, msanii Issa (2022) anaendelea kuielimisha jamii kwa kutoa nasaha za kujinga dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa korona. Msanii anaimba kama ifuatavyo:

> Masharti tufateni, yote tuliyowekewa
> Mikono isafisheni, kwa sabuni kutumia
> Mikusanyiko tuacheni, siyo lazima kukaa

Katika beti hizo (mfano wa 2 na wa 3) hapo juu, tunabaini kuwa kasida hujikita katika kutoa elimu muhimu ihusuyo korona. Wasanii wanaikumbusha jamii kufuata ushauri wa wataalamu wa afya. Wanakwenda mbali zaidi na kutaja njia muhimu za kufuata ili mtu asipate UVIKO 19. Njia hizo ni pamoja na kuepuka mikusanyiko na kunawa mikono kwa sabuni. Hii imetokea baada ya kubaini mambo yanayoweza kufanywa ili kujikinga na ugonjwa wa UVIKO-19 kama ilivyosisitizwa kwenye nadharia ya uhalisia kuwa msanii hujitahidi 'kuyachora' maisha jinsi yalivyo bila kuathiriwa; na hufanya hivyo kupitia vipengele muhimu vya maisha kama vile siasa, uchumi, utamaduni na jamii. Kwa hiyo, watunzi wa kasida wamefanya jukumu lao la msingi kwa kutumia kalamu na sauti zao kuielimisha jamii ili ifahamu kuhusu UVIKO-19. Ni wazi kuwa njia hizi ni katika njia muhimu zilizosisitizwa sana na wataalamu wa afya katika kuepuka maradhi haya (WHO, 2021). Hivyo, wasanii wanapozisisitiza ni wazi kuwa wanaitaka jamii izingatie maelezo ya wataalamu wa afya. Pia, kasida inagusia kitu muhimu pale inaposema "tujue wazi dawa haijapatikana". Hii ni elimu muhimu kwa wasikilizaji kuwa kuna umuhimu zaidi wa kujikinga na UVIKO-19 kwa kuwa dawa yake haijapatika. Kwa kuzingatia kuwa utungo huu ulitoka mwanzoni kabisa mwa mlipuko wa maradhi haya. Hivyo basi, kasida ilikuwa muhimu sana katika mapambano dhidi ya UVIKO-19.

### 4.3 Kueleza Hali ya Upatikanaji wa Huduma za Afya

Kasida hueleza hali ya upatikanaji wa huduma za afya kuhusu kuwapo kwa vituo vinavyosimamia afya za wanajamii. Vituo hivyo vinatarajiwa kuwa na wataalamu wa fani na mambo mbalimbali kuhusu afya. Kuwapo kwa vituo na wataalamu huwezesha upatikanaji wa huduma za afya na hivyo kuchangia kwa kasi ya

kupambana na janga la UVIKO-19. Msanii Issa (2022) katika kasida iitwayo *Korona,* anaendelea kusema:

Hili kwetu janga kubwa, ambalo limetokea
Limeondosha haiba, pembe zote za dunia
Nchi yetu masikini, bado haijaendelea
Itaweza kuhimili, gonjwa hili likienea

Katika ubeti huo, msanii anabainisha hofu kuhusu hali ya huduma za afya nchini. Msanii anaona kuwa yapo maeneo yenye umasikini uliokithiri na bila shaka maeneo hayo yana mifumo dhaifu ya upatikanaji wa huduma za afya. Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (2021), nchi za Afrika, zikiwamo Tanzania Bara na Zanzibar, zina mifumo dhaifu ya huduma za afya. Hali hiyo inaonesha kuwa bado upatikanaji wa huduma za afya hasa katika maeneo ya vijijini nchini upo chini. Aidha, katika maeneo ya mijini, huduma za afya ni za gharama kubwa na wanajamii wengi hawatumii bima ya afya ambazo zingerahisisha gharama za huduma za afya. Hivyo, kupitia kasida hiyo, msanii anatoa himizo kwa wananchi kufuata maelekezo ya wataalamu ili kuzuia kusambaa kwa UVIKO-19. Msanii anahitimisha kasida yake kwa kuihimiza jamii kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya. Hii ni kwa sababu ikiwa jamii itaacha kufuata maelekezo ya wataalamu basi ugonjwa utasambaa na kutatiza zaidi utoaji wa huduma za afya.

Hoja ya hali ya upatikanaji wa huduma za afya inafafanuliwa vyema na nadharia ya uhalisia kupitia msingi (d) unaoeleza kuwa mandhari na matukio inafaa yawe ni yale yanayoonekana, yanayojulikana au yanayowezekana. Inafaa mambo hayo yaendane na jamii husika. Hivyo, ni dhahiri kuwa mandhari ya jamii ya mwandishi inadhihirisha umasikini wa wanajamii kiasi cha kukosa mahitaji ya kumudu huduma chache za afya zilizopo na kwamba hali ya upatikanaji wa huduma za afya ni kikwazo katika kupambana na janga la UVIKO-19. Kwa ujumla, huu ni mtazamo mzuri na wa kiweledi kutoka kwa msanii.

## 4.4 Kubainisha Athari za UVIKO-19

Kasida pia zina mchango wa kubainisha athari nyingi zilizosababishwa na ugonjwa wa UVIKO-19. Wakati ugonjwa huo ulipoibuka na kusambaa duniani ilikosa amani na kila mtu alijawa na hofu na kiwewe. Msanii aliwasilisha hali hiyo kupitia kasida iliyobeba maudhui ya kueleza huzuni iliyoikumba jamii. Kasida ya *Korona,* msanii Ismail (2021) anaghani kama ifuatavyo:

Furaha waja hatuna, sote tunalia
Kwa maradhi ya Korona, yaloikumba dunia (x2)
Korona imeshaua, watu wengi kweli kweli
Tena inaendelea, kila kona kuathiri
Uchumi yashusha, inaweka ngumu hali
JUWAZA wahimiza, nasi Afanania
Tuliyokatwaza, tusijejifanyia

Katika mfano huo, tunabaini mambo matatu muhimu katika kasida hii. Mosi, janga la UVIKO-19 limezua hofu kwa jamii na kuwafanya kukosa raha na furaha katika maisha. Pili, janga la UVIKO-19 limesababisha vifo kwa wanadamu duniani kote. Hii ni kusema kuwa janga la UVIKO-19 limeua watu ndani na nje ya Tanzania. Vifo hivi vimezua taharuki, masikitiko na madhila kwa jamii. Mwisho, msanii anafafanua kuwa, janga la UVIKO-19 limeporomosha uchumi wa nchi na kuongeza umasikini kwa watu. Msanii anachosema hapa ni kuwa vifo vilivyotokana na UVIKO-19 siyo tu vimezua hofu bali pia vimeondosha nguvu kazi muhimu katika sekta mbalimbali za viwanda, afya, na elimu. Kuondoka kwa nguvu kazi hii kumeleta hasara kubwa kwa uchumi wa nchi na dunia kwa jumla.

Hoja hizo zinaonesha namna janga la UVIKO-19 lilivyo na athari mkubwa kwa mtu mmojammoja, taifa na dunia kwa ujumla. Katika kasida hii, msanii anasadifu nadharia ya uhalisia katika msingi (d) unaoeleza kuwa msanii hujitahidi ‘kuyachora’ maisha jinsi yalivyo bila kuathiriwa; na hufanya hivyo kupitia vipengele muhimu vya maisha kama vile siasa, uchumi, utamaduni, jamii pamoja na msingi unaoeleza kuwa msanii huangalia matatizo ya jamii na kuchunguza chanzo chake. Huchunguza mabadiliko ya kihistoria ambayo husababisha hali mbalimbali za maisha, ikiwa ni pamoja na kuathiri mifumo ya fikra. Kwa hakika, msanii ameonesha matatizo halisi yaliyosababishwa na janga la UVIKO-19 pamoja na athari mbalimbali za janga hili katika nyanja zote za kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii. Kwa ujumla, wasanii kupitia kasida hizo wanabainisha kuwa ugonjwa wa UVIKO-19 ulizua taharuki, woga na huzuni kubwa kwa wanajamii. Kila mmoja anafahamu namna habari za UVIKO-19 zilivyozua hofu na taharuki. Sambamba na kusababisha vifo vya watu na kuacha athari katika familia.

## 4.5 Kufanya Maombi Juu ya Kutokomeza UVIKO-19

Kutokana na janga hili lilivyoikumba jamii, kila mmoja kwa imani yake alimuelekea Mungu kumuomba kuwaondoshea balaa hili. Kwa upande wa watunzi wa kasida, mlipuko wa UVIKO-19 uliwasukuma kuandaa kazi zao kulingana na muktadha wa wakati huo. Ukiitazama hali hii kwa jicho la nadharia ya uhalisia ni wazi kuwa wasanii wamejibu kiu ya hadhira yao. Kwa kuona hali ilivyokuwa, ndiyo maana wasanii walitunga kasida zenye maudhui ya kuomba kwa Mungu kuwakinga wasipatwe na ugonjwa huo na kuwaponya wagonjwa. Pamoja na mambo mengine, tungo nyingi za wakati huo wa UVIKO-19, zililenga kuwapa wanajamii faraja na kuwakumbusha kuomba na kumtegemea Mola aliye juu ya kila kitu. Msanii Issa (2021) katika kasida yake inayojulikana kwa jina la “*Korona*” anasema maneno yafuatayo:

Mola tukinge nayo, maradhi Korona
Zitulie zetu nyonyo, maradhi Korona

Kwa wale walionayo, maradhi Korona
Wapone maradhi hayo, maradhi Korona

Vilevile, maudhui kama hayo kuhusu kufanya maombi yalijitokeza katika kasida mbalimbali zilizochunguzwa na mwandishi. Hayo yanajitokeza vema katika kasida iliyoimbwa na Nassor na Is-hak (2021) katika kasida yao iitwayo *Korona*, wasanii wanasema:

Tulinde Mola na hili janga la Korona, ulipeperushe kwetu lisije tena
Duniani kote, twateseka, tulinde wajao, twateseka
Uzilinde nchi, Zanzibari, Tanzania

Twamuomba Mola, Mola wetu Mwenye Enzi
Aondoe janga hili, kwa yake mapenzi
Maradhi yatia uduwanzi, hata pia na majonzi
Tuchukue tahadhari, atuepushe Mjuzi

Nchi zilopata pigo, hazitosahau katu
Tuepushe huu mzigo, nasi kwa upande wetu
Janga limeshatukwaza, na sasa limeenea

Swala hili twaliwaza, vipi tutalitatua
Mola pekee Muweza, yeye ndiye atambua
Vipi taliangamiza, tiba tukajipatia

Aidha, msanii Issa (2021) katika kasida yake iitwayo "*Korona*" anafanya maombi maalumu kwa Mwenyezi Mungu kwa kusema yafuatayo:

Tuondoshee ya Qadiru
Korona ulimwenguni
'Metukuka ya Baswiru
Yalatwifu ya Khabiru

Katika mifano hiyo tunabaini kuwa kasida zote zinasisitiza umuhimu wa maombi kama njia ya kulikabili janga la UVIKO-19. Wasanii wanahimiza waumini kujirejesha kwa Mungu na kuomba kinga yake ili wasalimike na ugonjwa wa UVIKO-19. Aidha, wasanii wanaonesha kuwa hatari ya ugonjwa ni kubwa na kuwa jamii imechanganyikiwa na haina pa kushika bali njia ya kweli ya kujizuia na hatari hii ni kumtegemea Mungu. Kwa kuutazama muktadha wa jamii iliyokusudiwa (Zanzibar) ambapo watu wake wengi ni Waislamu, ujumbe wa msanii ulikuwa muafaka na bila shaka ulipokelewa vema. Hivyo basi, wasanii wamesukumwa na muktadha wa jamii yao na wamewapa tiba kulingana na mahitaji halisi ya jamii. Hii ni kusema kuwa msingi wa Uislamu kama zilivyo dini nyingine kuu zilizo Afrika unahimiza waumini kumtegemea Mungu na kumuomba msaada wakati wa madhila/majanga. Watunzi wa kasida hizi wametoa mchango mkubwa kwa kuhusisha kazi zao na matukio yaliyomo katika maisha ya kila siku.

Kiukweli, watunzi wametumia lugha ya maombi ili wanajamii waweze kupata kinga kutokana na janga la UVIKO-19. Hivyo basi, wasanii kupitia kazi zao wamewakumbusha wanajamii kumuomba Mungu ili awasaidie kuondokana na balaa la ugonjwa wa UVIKO-19.

## 5.0 Hitimisho

Makala hii imebainisha mchango wa kasida teule za Zanzibar katika mapambano dhidi ya UVIKO– 19. Kwa muhtasari, kasida zimetoa elimu kwa jamii kuhusu janga la UVIKO-19. Kwanza, kasida zimesaidia kutoa elimu wakati muafaka kulingana na mahitaji ya wakati huo ambapo wanajamii walihitaji sana maneno ya faraja kutoka katika vinywa na kalamu za wanafasihi. Pili, kasida zimezungumzia mambo mengi muhimu na yenye manufaa kwa jamii. Kasida zote zilizorejelewa katika makala hii zimegusa karibu maeneo yote kuhusu janga la UVIKO-19, hivyo kuinufaisha jamii. Tatu, watunzi wamezingatia kwa kiasi kikubwa muktadha wa kijamii katika kufikisha ujumbe wao. Hii ni kusema kuwa jamii ya Wazanzibari ambao wengi ni Waislamu wamenufaika zaidi na ujumbe wa utanzu wa kasida kwa kuwa ni utanzu wa "nyumbani" unaotumika sana visiwani Zanzibar kwa ajili ya kufikisha ujumbe kwa jamii. Katika kufanya hivi, watunzi wameusawiri uhalisia wa maisha ya wanajamii katika kipindi cha janga la UVIKO-19 na hivyo kuwezesha matumizi ya nadharia ya uhalisia katika kufanikisha utafiti wa makala hii.

## Marejeleo


BAKIZA (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. Cambridge: OpenBook Publishers.

Ismail, A. (2021). (Mtunzi). *Korona.* Imetazamwa 15.04.2022, kutoka https://youtu.be/Oooon 6LZSJV8.

Issa, A. (2021). (Mtunzi). *Korona.* Imetazamwa tarehe 16.04.2022, kutoka https://www. youtube.com/watch?v=kDT0MtNFPZg.

M'barouk, F. (Mtunzi). (2021). *Turejee kwa Allah*. Imetazamwa tarehe 11.04.2022, kutoka https://www.youtube.com/watch?v=Tad8u1qbe6E.

Mlaga, W. K. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Karne ya 21*. Dar es Salaam: Heko Publishers Ltd.

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*, Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*, Rock Island: Augustana College.

Said, S. S. (2016). Maana na Mafunzo Yanayopatikana katika Nyimbo za Michezo ya Watoto Wadogo Zanzibar. Tasnifu kwa Ajili ya Shahada ya Kwanza. Chuo Kikuu Cha Taifa SUZA. (Haijachapishwa).

Shekhe Issa (2022). (Mtunzi). *Korona.* Imetazamwa 16.04.22, kutoka https://youtube.be/ 1XFlhX_hVas.

Wafula, R. M. & Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation..

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi*: *Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publication Ltd.

WHO (2021). WHO Strategic Action against COVID-19: 2021 Mid-Year Report: WHO: Geneva.